# TUNDUMA MPYA YA MAENDELEO

JARIDA MAALUMU MWEZI SEPTEMBA




*Mbio za mwenge wa Uhuru 2022 Halmashauri ya Mji Tunduma*





Mkuu wa Wilaya ya Momba Mhe. Fakii Lulandala akipokea Mwenge wa Uhuru toka kwa Mkuu wa Wilaya ya Ileje tarehe 17-9-2022





Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru 2022 Halmashauri ya Mji Tunduma





*Wananchi wa Halmashauri ya Mji Tunduma tumeungana na Watanzania wenzetu kutekeleza ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 usemao:*

***"Sensa ni msingi wa Mipango ya Maendeleo: Shiriki kuhesabiwa, tuyafikie Maendeleo ya Taifa''***

*Sambamba na kaulimbiu hii, Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022, zinaendelea kuhamasisha wananchi kupambana na*

***"Rushwa, Dawa za Kulevya, VVU/UKIMWI, Malaria na kuwaelimisha Wananchi juu ya Lishe Bora kwa Afya Imara."***



*Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2022 umekimbizwa kwa jumla ya kilomita 38 na kupitia miradi ya maendeleo **8** yenye thamani ya*
***sh. 3,110,974,213.70** Kati ya fedha hizo:-*

***Fedha kutoka Serikali Kuu ni kiasi cha sh. 816,322,725.00/=***
***Mapato ya ndani ya Halmashauri ni sh 895,883,364.73/=***
***Michango ya nguvu za wananchi ni sh. 24,396,000.00/=***
***Wahisani, UVIKO 19 na TOZO ni sh. 1,004,039,499/=***

*Mwenge wa uhuru mwaka 2022 umezindua miradi miwili **(2),** umeweka jiwe la msingi miradi mitatu **(3)** na mradi mitatu **(3)** imekaguliwa. Miradi hii iko katika sekta za Ardhi na Mipango miji, Afya, Maji, Elimu, Barabara, na Maendeleo ya Jamii*

# MRADI WA KWANZA: UZINDUZI WA UPIMAJI ARDHI






**GHARAMA YA MRADI**

Mradi huu umetekelezwa kupitia Fedha za Mkopo usio na riba wa Sh. 543,000,000/= uliotolewa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kiasi cha fedha kilichotumika mpaka sasa katika kukamilisha mradi huu ni Sh. 535,416,591.20. Kiasi cha Sh 7,583,408.80 kilichobaki kitatumika katika kuboresha miundombinu ya eneo lote lenye jumla ya ekari 155



Mkuu wa Divisheni ya Ardhi Adbul Mbwana akisoma taarifa ya Mradi wa viwanja

**MANUFAA YA MRADI**

Kutokana na mauzo ya viwanja hivi, Halmashauri ya Mji inatarajia kukusanya jumla ya Sh.1,066,974,242/=, ambazo kati ya hizo Sh. 543,000,000/= zitarejeshwa Serikali Kuu ili kulipa mkopo uliotolewa bila riba na kuifanya Halmashauri ya Mji kupata mapato ya kiasi cha Sh. 523,974,242/= kama faida na kuweza kutumika katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya Mji wa Tunduma.







MUONEKANO WA RAMANI YA MRADI WA UUZAJI WA VIWANJA MSINDE

# MRADI WA PILI: KUKAGUA KLABU YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA






Klabu ilianzishwa mnamo mwezi Julai, 2008 na Kuzinduliwa rasmi na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, mwaka 2010 Dr. NASSORO ALLY MATUZYA tarehe 29/08/2010 ikiwa na jumla ya Wanachama 81 kati ya hao Wavulana walikuwa 68 na Wasichana 13 wote wakiwa ni Wanafunzi wa kuanzia Kidato cha I hadi cha IV kwa wakati huo. Kwa sasa Klabu yetu ina jumla ya Wanachama 120 ambapo wavulana ni 40 na wasichana ni 80, wote wakiwa ni kuanzia Kidato cha I hadi cha VI.

MANUFAA YA MRADI

Madhumuni ya kuanzisha Klabu hii ni pamoja na kutumia nafasi yetu kama Wanafunzi kushiriki katika vita dhidi ya rushwa. Kwa kuwa mapambano dhidi ya rushwa si jukumu la Serikali kupitia TAKUKURU peke yake, bali ni jukumu la kila mmoja wetu. Tunashiriki kwa kuwaelimisha Wanafunzi wenzetu, Wazazi/Walezi wetu na jamii kwa ujumla juu ya athari za rushwa na wajibu wao katika vita hivi dhidi ya rushwa. Elimu hii tunaitoa kupitia Sanaa ya nyimbo, maigizo, mashairi pamoja ugawaji wa machapisho. Pia hufanyika kwa njia ya mijadala na midahalo baina yetu Wanafunzi hapa shuleni.





Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022, Sahili Nyanzabara Geraruma akikagua kazi za klabu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

*Wanaklabu wanapenda kuwaasa Viongozi na Wananchi wote kuzingatia na kutekeleza kwa vitendo ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu 2022 chini ya kauli mbiu **"Kuzuia Rushwa ni Jukumu langu."** Ikiwa kila mmoja wetu ataamua kwa dhati kupambana na rushwa kwa kuikataa kwa dhati, kutotoa wala kupokea rushwa pamoja na kuwafichua wale wanaojihusisha nayo, tutaweza kupunguza kama siyo kumaliza tatizo hili hapa nchini*



*KLABU YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA*




# MRADI WA TATU: UJENZI WA KITUO CHA AFYA MWAKAKATI






Utekelezaji ulianza rasmi 01/03/2022 kwa ujenzi wa jengo la OPD, jengo la Maabara na kichomea taka. Majengo ya mama na Mtoto, upasuaji na jengo la kufulia ujenzi wake ulianza 01/06/2022. Muda uliopangwa kukamilisha mradi 14/04/2022 kwa jengo la Maabara, 29/04/2022 kwa jengo la OPD na 30/07/2022 kwa majengo ya mama na mtoto, upasuaji na jengo la kufulia





Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022, Sahili Nyanzabara Geraruma akikagua Ujenzi wa Kituo cha Afya Mwakakati

GHARAMA ZA MRADI

Fedha iliyopokelewa kutoka chanzo cha TOZO za miamala ya simu ni sh 500,000,000/= kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mji Tunduma sh 31,990,498/= na sh. 12,450,000 ni thamani ya nguvu za wananchi hivyo kuufanya Mradi kuwa na thamani ya sh. 544,440,498/=





Muonekano wa Jengo la wagonjwa wa Nje (OPD) wa Kituo cha Afya Mwakakati


# MRADI WA NNE: UZINDUZI WA MRADI WA MAJI






**GHARAMA ZA MRADI.**

Fedha iliyotengwa kama gharama za mradi huu ni **Sh. 876,753,123.97,** ambapo **Sh. 504,039,499.01** ni fedha za UVIKO-19, **Sh. 370,032,623.96** ni fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji na **Sh. 2,681,000** ni thamani ya nguvu za wananchi. Hadi sasa jumla ya shilingi **506,441,288.56** zimetumika kwa kumlipa mkandarasi na ununuzi wa vifaa. Fedha iliyobaki ni **Sh.370,311,834.41**






**MANUFAA YA MRADI.**

Mradi huu utaongeza upatikanaji wa Maji Safi na salama kwa wananchi wapatao 23,261 na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia 9.8 kutoka asilimia 65.45 mpaka kufikia asilimia 75.25 katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma.





# MRADI WA TANO: UWEKAJI JIWE LA MSINGI MADARASA YA GHOROFA






**GHARAMA ZA MRADI.**

Jumla ya makadirio ya gharama za mradi ni **Sh. 829,637,866.73**. Kati ya hizo **Sh. 820,372,867/=** ni fedha za mapato ya ndani toka Halmashauri ya Mji Tunduma na **Sh. 9,265,000/=** ni michango ya wananchi






**MANUFAA YA MRADI.**

a. Itapunguza kwa kiasi kikubwa msongamano na mrundikano wa wanafunzi darasani na kuongeza ufanisi katika ufundishaji utakaopelekea kuinua kiwango cha elimu ambao utaleta manufaa katika ukombozi wa jamii kifikra, kimtazamo na mwisho kuchochea ustawi na uchumi wa taifa.

b. Mradi huu pia utakua dira na kutatua changamoto mpya za kimapinduzi katika sekta ya elimu hasa ya msingi, katika ukanda na mkoa wetu, kwamba serikali inayo nia na dhamira ya dhati katika kuboresha mazingira na miundombinu ya elimu kama ilivyoelekeza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 sehemu ya tatu ibara ya 80.





# MRADI WA SITA: UZINDUZI WA MRADI WA BARABARA ZA LAMI






Miongoni mwa barabara zilizofanyiwa maboresho ni Victoria - Mbambila km 0.34, Sichembe km 0.05 na Kampala km 0.11. Utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi tarehe 23/08/2021 na ulikamilika tarehe 23/04/2022.





GHARAMA ZA MRADI

Mradi huu umegharimu kiasi cha Sh.273,322,725 /= Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami mita 500, Ujenzi wa mifereji mita 913 na Ujenzi wa kalvati mistari mitatu(3)



# MRADI WA SABA: UKAGUZI WA MRADI WA VIJANA WALIONUFAIKA BODABODA






Gharama za Mradi

Katika kituo chetu cha mradi wa usafirishaji kwa njia ya Pikipiki tunazo pikipiki 16 ambazo zimegharimu kiasi cha Sh 43,200,000/=.





Manufaa ya Mradi

i. Mkopo huu wa pikipiki umetupatia ajira za kudumu
ii. Kupitia mradi wa uendeshaji wa pikipiki tumeweza kupata mafunzo ya udereva na usalama barabarani ambayo wengi wetu hatukuwa nayo awali
iii. Kutokana na mkopo huu tumeanza kufanya marejesho ya Mkopo Halmashauri kwa wiki, ambapo kila wiki pikipiki moja inarejesha Sh 56,250/=
iv. Kupata mafanikio ya kubaki na kiasi cha Sh 13,000/= hadi Sh. 15,000/= kwa siku na kwa mwezi tuna uhakika wa kupata Sh. 420,000/=, ukitoa matumizi ya familia tunaweza kubakiza kati ya Sh100,000/= hadi Sh 150,000/=



# MRADI WA NANE: UKAGUZI WA AFUA ZA LISHE






GHARAMA ZA MRADI

Gharama za mradi ni sh. 320,000,000 ambazo ni fedha toka mapato ya ndani ya Halmashauri.





MAFANIKIO YA KIKUNDI.

Kwa kipindi cha 2021/2022 jumla ya watoto 1,787 wenye umri kuanzia miezi 0-59 walipimwa hali zao za lishe katika kata ya Chipaka, Vipimo hivi vilifanyika kwa kutumia kipimo cha mzingo wa mkono (MUAC TAPE). Kati ya watoto wote waliopimwa matokeo yanaonyesha watoto 12 walikuwa na utapiamlo wa kati, 2 walikuwa na utapiamlo mkali. Watoto hawa waliunganishwa katika vituo vya matibabu na wanaendelea kupata matibabu stahiki. Elimu ya unasihi juu ya ulaji unaofaa kwa wazazi wa watoto hawa ilitolewa na kikundi ikiongozwa na watoa huduma wa Afya kwenye mitaa.



*Tunawashukuru na kuwapongeza sana wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2022 wakiongozwa na **Sahili Nyanzabara Geraruma** kwa umahiri wao katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kutuwasilishia ujumbe wa Mwenge wa Uhuru ambao tunaahidi kuutekeleza kwa vitendo, juhudi na nguvu zote.*

*Mwenge wa uhuru mwaka 2022 umezindua miradi miwili **(2),** umeweka jiwe la msingi miradi mitatu **(3)** na mradi mitatu **(3)** imekaguliwa. Miradi hii iko katika sekta za Ardhi na Mipango miji, Afya, Maji, Elimu, Barabara, na Maendeleo ya Jamii*

*HAKUNA MRADI ULIOKATALIWA NA WAKIMBIZA MWENGE WA UHURU 2022 KATIKA HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA*









# Asante Mwenge wa Uhuru 2022




# *Kwaheri Mwenge wa Uhuru 2022*



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma Philemon Magesa akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba Bi. Regina Bieda